

UTANGULIZI

MAMBO 3 KUHUSU MAISHA KATIKA ULIMWENGU ULIOANGUKA

1. Majaribu hayawezi kuepukwa.

Wapenzi, msione kuwa ni ajabu ule msiba ulio kati yenu, unaowapata kama moto ili kuwajaribu, kana kwamba ni kitu kigeni kiwapatacho. (1 Petro 4:12)

Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu. (Yohana 16:33)

Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa. 13 Lakini watu waovu na wadanganyaji wataendelea, na kuzidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika. (2 Timotheo 3:12-13)

2. Majaribu "hutujenga" au "hutuvunja."

3. Waathiriwa hushindwa kufanya lolote zaidi ya kuuliza "kwa nini" na wanabaki wamekwama katika maumivu yao.

NENO KUTOKA KWA MUNGU KWA WALE AMBAO MAISHA YAO "YANASAMBARATIKA."

Yakobo, mtumwa wa Mungu, na wa Bwana Yesu Kristo, kwa makabila kumi na mawili waliotawanyika; salamu. Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno. (Yakobo 1:1-4)

1. Je, naweza kudhibiti nini maisha yangu yanaposambaratika?

Jibu: MTAZAMO WANGU (Yakobo 1:2)

"Hesabuni" – tathmini, hesabu, chagua

"Furaha tupu" – mtazamo = kimsingi "ambayo haijachanganywa na chochote, au furaha kamili"

"Majaribu" – kuzungukwa na

2. Je, napaswa kufanya nini ili niweze kuipita siku ya leo vizuri?

Jibu: VUMILIA (Yakobo 1:3)

"Kujua" – kwa kupitia matukio fulani = mtazamo

"Kujaribiwa" – kuidhinisha, kutakasa, kuonyesha kuwa ni halisi

"Uvumilivu" – hupo-meno = nguvu ya kusalia imara

3. Je, nina tumaini gani kwa ajili ya kesho?

Jibu: Mungu atachukua kile kilicho KIBAYA ZAIDI na kukitumia kuniletea kile kilicho BORA ZAIDI. (Yakobo 1:4)

"Saburi na iwe" – ruhusu, shirikiana na kazi ya Mungu ili uweze kuwa...

"Kamilifu" – mkomavu, mbivu, kukua kikamilifu

"Watimilifu" – kamili, yenye sehemu zilizoumbika vyema na kukomaa, isiyopungukiwa na chochote

JINSI MUNGU ANAVYOTUMIA DHIKI KUTUKOMA ZA

1. Tunalazimika KUMTEGEMEA Mungu katika kiwango kipya. Tukiachwa kuishi tunavyotaka, tunakuwa na mwelekeo wa kujitegemea wenyewe, kuwa na kiburi, na kutomjali Mungu.
2. TUNAONDOLEWA kutoka kwenye mambo ya maisha ya muda mfupi, ya dharura na ya kidunia. Tunalazimika KUCHUNGUZA UPYA maadili, vipaumbele, majukumu na mustakabali wetu.
3. Majaribu HUTUWEZESHA kushuhudia moja kwa moja uhalisia na nguvu ya Mungu. Mahitaji yetu yanakuwa chombo cha kuonyesha neema ya Mungu; matatizo yetu yanakuwa lengo la nguvu yake.
4. Majaribu hutumika kama USHUHUDA mzuri sana kwa ulimwengu usioamini. Jinsi tunavyovumilia dhiki huonyesha ulimwengu jinsi Mungu alivyo halisi.
5. Tunakuwa watu WANA OIGA MFANO WA KRISTO ambao ni wenye kuzingatia hisia za wengine, wenye kujali na wenye huruma. Wale ambao wameumizwa sana huwa na mwelekeo wa kuwa na upendo sana.

MASWALI YA MAJADILIANO

1. Shiriki hali mbaya ambayo ulipitia maishani mwako hapo nyuma ambayo (ingawa ilikuwa ngumu) imekuwa na matokeo mazuri katika maisha yako.
2. Ingawa ni jambo la kawaida sana, kwa nini ni muhimu kuenda zaidi ya kuuliza "kwa nini?"
3. Je, ni hali gani katika maisha yako ya sasa ambayo inastahili kuitwa jaribu, au "hali ya kusambaratisha maisha"?
4. Chukua muda na upitie maswali matatu ya "nini" ambayo Mungu anatupatia katika Yakobo 1:2-4.
5. Jadili jinsi unavyoweza kutekeleza ukweli huu katika hali yako ya sasa. Fungeni kwa kuwa na muda wa kushikana mikono na kuomba.